SURA YA NNE

Hoja ya Shirikisho na Siasa za Tanzania

Rasul Ahmed

Utangulizi

Mnamo Mei 30, 2005 mjini Dar es Salaam, Wakuu wa nchi tatu zilizoasisi Jumuiya ya Afrika Mashariki, Benjamin William Mkapa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Yoweri Kaguta Museveni wa Jamhuri ya Uganda na Mwai Kibaki wa Jamhuri ya Kenya waliupitia tena uamuzi wa Mkutano wao usio wa kawaida uliofanyika mjini Nairobi tarehe 28 Agosti, 2004 na kuamua kuunda kamati ya kuangalia namna na njia ya kuharakisha na kufupisha mchakato wa ushirikiano ili hatimaye lengo la kuunda shirikisho litimizwe. Katika mkutano huo wakuu wa nchi hizo tatu walisisitiza tena kuunga mkono wazo la kuharakisha shirikisho. Wakuu hao pia walitambua kuwa shirikisho imara litawezekana tu kama litamilikiwa na wananchi wa Afrika Mashariki wenyewe kwa kushirikishwa ipasavyo kuanzia hatua yake ya mwanzo mpaka mwisho. Hivyo basi, wakasisitiza haja ya kutanua uwanja wa mashauriano ili kushirikisha wadau wote muhimu. Ili kufanikisha hilo waliziagiza nchi husika kuunda kamati za kukusanya maoni. Mchakato wa kukusanya maoni ulizinduliwa kwa pamoja katika miji mikuu ya nchi hizo tatu mnamo Oktoba 13, 2006. Ni kwenye mkutano huo ndipo Wakuu hao wa nchi walipokubaliana kuteua Mawaziri

watakaoshughulikia masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kama njia mojawapo ya kuharakisha mchakato wa ushirikiano kuelekea shirikisho la Afrika Mashariki.

Kwa mara nyingine tena, hoja ya Shirikisho la Afrika Mashariki limechukua nafasi kubwa hivi sasa katika duru za kisiasa za ndani ya nchi kama ilivyokuwa mwanzoni mwa miaka ya sitini wakati Tanganyika inapata uhuru. Kama ilivyothibitishwa na aliyekuwa Waziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki anayeshughulikia Fedha na Utawala, Al Noor Kassum (1977), miaka ya mwanzo ya uhuru wa nchi za ukanda huu ulishuhudia mazungumzo kuhusu shirikisho yakifanyika katika mabaraza mbalimbali, marais na mawaziri wakuu walikutana, wabunge walikusanyika pamoja kuzungumza, na vyama vya siasa viliitisha mikutano ya hadhara. Ali mradi kulikuwepo na tumaini kubwa la kumaliza matatizo yaliyokuwepo na hatimaye kuunda Shirikisho mara moja. Kwa hakika, muktadha wa kisiasa wa wakati ule ni tofauti kabisa na ulivyo leo hii. Muktadha wa kisiasa wa miaka ya sitini uliruhusu wadau wa mfumo wa kisiasa wakati huo wakiongozwa na watawala na wanasiasa kuhimiza mara kwa mara kuunda moja kwa moja Shirikisho bila kuwa na haja ya kuunda aidha Tume au Kamati ya kukusanya maoni ya wananchi. Mabadiliko ya muktadha wa kisiasa yaliyoanza kuchomoza kuanzia mwongo uliopita, na ambayo yamechangiwa na mabadiliko ya uendeshaji wa mifumo ya kisiasa, kiuchumi na kisheria, yameainishwa na sifa kuu moja, miongoni mwa sifa nyingine: kuweka utaratibu wa kukusanya maoni ya wananchi kabla ya kufanya maamuzi makubwa kama kubadilisha mfumo wa kisiasa, kubadili katiba na sasa kuharakisha shirikisho.

Si lengo la makala hii kufanya tathmini ya jinsi na kwa ustadi gani maoni ya wananchi yamekuwa yakikusanywa na kufanyiwa kazi. Makala hii inatazama hoja hii ya Shirikisho la Afrika Mashariki ikilinganisha na duru za kisiasa za Tanzania. Ili kutimiza hilo makala hii imegawanywa kwenye sehemu sita. Baada ya utangulizi huu sehemu inayofuata inatoa muhtasari wa hali ya siasa ilivyo pamoja na mitazamo dhidi ya Shirikisho kwa kuzingatia historia. Sehemu ya tatu inatafakari nafasi ya Serikali kuu chini ya tawala tofauti katika masuala ya Jumuiya. Hii inafuatiwa na mjadala

unaokutanisha vyama vya siasa, wanasiasa na masuala ya Jumuiya kwa ujumla. Sehemu ya tano itagusia mitazamo kuhusu visiwa vya Zanzibar na mahusiano yake na hoja ya Shirikisho. Sehemu ya sita inatoa hitimisho.

Hali ya Kisiasa Ilivyo Tanzania

Kabla ya kuchambua mada kuu ya makala hii ni vyema kutazama hali ya siasa ilivyo nchini kwa ujumla. Kwa muhtasari, Tanzania ina mfumo wa kisiasa wa vyama vingi tangu 1992. Mfumo huu ambao una takribani zaidi ya miaka 14 unaweza kuelezewa na mambo kadhaa muhimu. Hapa tunataja machache, nayo ni:

- Ushiriki rasmi katika siasa na chaguzi mbalimbali ni kupitia vyama vya siasa vilivyosajiliwa na ofisi ya msajili wa vyama. Katika siku za hivi karibuni suala la wagombea binafsi ambalo lilikatazwa kwenye mabadiliko ya nane ya katiba liliibuka mahakamani na kuamuliwa wakubaliwe kushiriki kwenye chaguzi. Taratibu za kuwezesha hilo kutokea bado hazijafanywa;

- Sambamba na hilo ni mfumo wa siasa 'kutawaliwa na utamaduni wa vyama vya siasa' [supremacy of political parties culture] kutokana na sheria ya vyama vya siasa kuvipa nguvu vyama vilivyosajiliwa (Nyirabu, 2002:106);

- Vyama vya siasa vilivyosajiliwa ni kumi na nane, lakini ni vitano tu vyenye uwakilishi bungeni;

- Nguvu ya vyama vya upinzani dhidi ya chama tawala imezidi kupungua baada ya kufanyika chaguzi tatu kuu. Ushindani wa kisiasa upo zaidi upande wa visiwani ambapo vyama vya CCM na CUF vina ufuasi mkubwa. Ilipofika Februari Mosi 2002 kambi ya upinzani katika Bunge la Jamhuri ya Muungano ulikoma kutambuliwa baada ya chama cha CUF kuwavua uanachama wabunge wake watatu kwa sababu za utovu wa nidhamu. Hali ya kuwa na Bunge ambalo wabunge wengi ni kutoka

chama kimoja imepelekea mchambuzi mmoja kusema kuwa nchi imerejea utawala wa chama kimoja (Wambali kama alivyonukuliwa na Nyirabu, 2002);

- Kama ilivyo kwenye mifumo ya kisiasa kwingineko barani kumekuwepo matukio ya viongozi na wanachama kubadilisha vyama. Huku kunafanyika kwa sura tatu, kama inavyobainishwa na Max Mmuya (2002): Sura ya kwanza ni Chama kizima kuhamia Chama kingine bila kuvunja Chama cha awali kimuundo na kiuongozi. Sura ya pili ni kwa viongozi wa upinzani wa ngazi mbalimbali kuhamia Chama tawala, na sura ya tatu ni uongozi wa vyama vya upinzani kuhamia vyama vingine vya upinzani. Hali hiyo ya kuhamahama ipo pia kwa wanachama wa kawaida. Mmuya anabainisha pia kuwa "mkondo mwingine ni wa vyama kumeguka na kujaribu kuunda vyama vipya;"

- Migogoro baina na ndani ya vyama vya siasa imekuwepo ambayo kwa kiwango fulani imetia doa wasifu wa siasa za ndani ya nchi;

- Masuala ya Katiba mpya na Tume Huru ya Uchaguzi yameendelea kuwa kilio cha wanasiasa wa kambi ya upinzani;

- Utafiti uliofanywa na mpango wa REDET mwaka 1994 kuhusu utamaduni wa kisiasa ulibainisha kuwa watu wana imani na chaguzi, isipokuwa Zanzibar, na kwa ujumla wanapendelea zaidi njia za amani kufikia suluhu za matatizo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa (Mushi, 2004);

- Na katika utafiti wa 2001 uliofanywa na Afrobarometer kwa ushirikianao na REPOA ulibainisha yafuatayo:

  - ikilinganishwa na nchi nyingine za Kiafrika, Watanzania wanaonyesha shauku kubwa ya kushiriki kwenye siasa na mikusanyiko ya kisiasa kama vile mikutano ya hadhara, kampeni na kupiga kura. Lakini wanaonyesha kiwango kidogo cha ushiriki binafsi katika siasa kama

vile kuwasiliana na viongozi wao wa kisiasa na kujiunga na vyama vya kijamii;

- Kwa ujumla watanzania wanaunga mkono demokrasia na kukataa njia mbadala zisizo za kidemokrasia;

- Ingawa watanzania wengi wanaonyesha kuridhishwa na namna demokrasia inavyokuwa, wanatambua bado nchi ina safari ndefu kuelekea demokrasia iliyokamilika; na

- Watanzania wanaonyesha ustahimilivu wa hali ya juu kuhusu michakato ya mageuzi ya kiuchumi na kisiasa. (Chaligha *et. al.*, 2002).

Hata hivyo, Watanzania kama walivyo wakazi wengine wa ukanda wa Afrika Mashariki wameonyesha kuwa na uelewa mdogo kuhusu shughuli za Jumuiya ya Afrika Mashariki kama ilivyobainishwa na Kamati ya Wako, na hivi karibuni Kamati ya Wangwe. Hali hiyo iliilazimu Kamati ya Wangwe kutoa elimu kwanza kuwawezesha wananchi kuelewa Kamati imetumwa kuhoji nini na shughuli nzima za Jumuiya kabla ya kukusanya maoni (Habari Leo, Aprili 8,2007).

Nguvu za Kisiasa na Mitazamo Dhidi ya Shirikisho Kihistoria

Ili kupata undani wa namna hoja ya shirikisho inavyohusiana na siasa za Tanzania hatuna budi kuirejea historia japo kwa muhtasari. Hapa tunawasilisha hoja kuwa tangu taifa hili linazaliwa, chini ya awamu ya kwanza ya uongozi wa nchi, duru za kisiasa zilionyesha kuthamini hoja ya Shirikisho la Afrika Mashariki. Uthibitisho wa hili ulijionyesha kwenye kauli, matamko na hata vitendo vya watawala wa nchi hii katika awamu zote nne za uongozi wa taifa hili, iwe katika duru za kisiasa za ndani au kimataifa.

Itakumbukwa kuwa juhudi za kuunganisha eneo la ukanda wa Afrika Mashariki zilianza wakati wakazi wa eneo hilo wakiwa bado chini ya tawala za kikoloni. Juhudi hizo zilizoanza mwishoni mwa karne ya 19 kwa kuanzisha miradi kadhaa iliyojaribu kuunganisha uchumi wa Kenya na

Uganda, na Tanganyika kujiunga mwanzoni mwa miaka ya 1920. Juhudi hizo ziliambatana na uanzishwaji wa taasisi na tume mbalimbali. Si lengo la makala hii kurejea kwa undani sana kilichotokea lakini kwa ufupi ni kwamba tangu kipindi hicho, ziliundwa tume kadhaa za kuangalia uwezekano wa kuwa na shirikisho la Afrika Mashariki. Tume hizo ni zile za Ormsby-Gore [1924], Hilton-Young [1927], na kamati ya pamoja ya Bunge la Uingereza [1931].

Wakati nchi za Tanganyika, Uganda na Kenya zinapata uhuru nusu ya mwanzo ya miaka ya sitini tayari ari ya kuwa na mshikamano wa kisiasa miongoni mwa Waafrika ulikuwa umeshika kasi (Tarrosy, 2005). Katika ukanda huu, baada ya Tanganyika kuwa nchi ya kwanza kupata uhuru mwaka 1961 shauku ya kuwa na shirikisho iliongezeka. Serikali ya Tanganyika huru ilikuwa tayari kuahirisha uhuru wake kwa mwaka mzima kama Uingereza ingetoa uhuru kwa Kenya na Uganda kwa wakati mmoja (Sebalu, 1972: 347).

Katika duru za kimataifa, kauli na vitendo vya Serikali vilithibitisha bila kuonyesha shaka yoyote kuwa nchi hii inaamini na kuthamini hoja za Shirikisho. Kuanzia masuala ya PAFMECA,[1] ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika, Umoja wa Afrika kupitia ushirikiano wa kikanda, duru za kisiasa zilionyesha kuunga mkono hoja za shirikisho huku watawala wakifikiria namna bora ya kugawana kwa usawa gharama na manufaa ya ushirikiano wa kikanda. Rais wa kwanza na mmoja wa waasisi wa taifa la Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliziona nchi za Afrika Mashariki zenye mwanya wa kipekee wa kuanzisha ushirikiano kutokana na kuwa na historia ndefu ya ushirikiano inayoanzia enzi ya ukoloni (Msambichaka *et. al.*, 2002:250 kama ilivyonikuliwa katika kitabu cha Tarrosy, 2005). Mwalimu Nyerere alisisitiza sana umuhimu wa kuunda Shirikisho la Ukanda wa Afrika Mashariki hata kabla ya uhuru wa nchi husika, huku akifananisha hoja ya bado kidogo na ile iliyokuwa ikitumiwa

[1] PAFMECA ambayo kirefu chake ni Pan-african Freedom Movement for East and Central Africa ilianzishwa mjini Mwanza, Tanzania, Septemba 1958, Tanzania ikatoa Katibu Mkuu wake wa kwanza.

na mabeberu kucheleweshe uhuru. Mwalimu alijua kuwa na shirikisho baada ya uhuru kamili itamaanisha kusambaratisha mamlaka ya dola, hivyo kama ilikuwa vigumu kuwashawishi marafiki zetu kuwa na Shirikisho kabla ya uhuru wakati ambao haliusishi kusalimisha mamlaka, itakuwa vigumu zaidi hapo baadaye (Nyerere, 1966). Kwa lugha ya Kiingereza Mwalimu alisema:

> [.....Federation after complete independence means the surrender of sovereignty and all the prestige and symbols of such sovereignty. Surely, if is difficult now to convince some of our friends that Federation is desirable, when it does not involve surrendering any sovereignty, it is going to be a million times more difficult to convince them later...]

Utabiri wa Mwalimu Nyerere ulithibitika baada ya kipindi kifupi. Mambo yalibadilika baada ya Uganda [1962] na Kenya [1963] kupata uhuru. Shauku ya kuwa na shirikisho la kisiasa ilififia hali iliyochangiwa na sababu za kisiasa za wakati huo. Tawala za wakati huo zilikuwa katika mapambano makubwa ya kujikirimisha kisiasa, wakati ambao ushikaji hatamu wa tawala hizo ulikuwa bado dhaifu na wakati huohuo changamoto za ujenzi wa nchi na uimarishaji wa mifumo ya utawala ilihitaji fokasi ya kitaifa (Mukandala na Killian, 2004:185). Mukandala na Killian wanabainisha kuwa tofauti na kutokufikia makubaliano kuhusiana na mgawanyo wa gharama na faida za ushirikiano lazima zitaangaliwa kwa mtazamo huo. Wanaendelea kusema kuwa hiki hakikuwa kipindi muafaka cha kufikia makubaliano yoyote ya maana kama ilivyothibitika kwa kushindwa kutekeleza vilivyo mapendekezo ya Tume ya Raisman [1961], Azimio la Nairobi [1963], Makubaliano ya Kampala [1964], na Tume ya Mawaziri [1965] [ibid.]

Ni vyema pia tukakumbuka utayari wa Tanzania kipindi hicho kujitoa mhanga kwa minajili ya kuhakikisha ndoto ya kuwa na Shirikisho la Afrika Mashariki hata pale maslahi yake kiuchumi yalipokuwa mashakani. Mwanzoni mwa mwaka 1964 aliyekuwa Waziri wa Masuala ya Nje wakati huo, Oscar Kambona alikaririwa akisema:

> "...Tulipopata uhuru 1961 tulikubali kuendelea na utaratibu uliokuwepo wa soko la pamoja, sio kwa kuamini kuwa ulikuwa ni wa haki na usawa, bali tulijiandaa kuuona kama hatua ya mpito kuelekea shirikisho. Kama shirikisho

lingeahirishwa kwa kipindi kisichojulikana, hata hivyo, tusingeweza kuendelea kupuuza mapungufu ambayo Tanganyika ilirithi kwenye soko hilo la pamoja...." [Tafsiri isiyo rasmi][2]

Ujumbe kama huo ulitolewa na Mwalimu Nyerere wakati akihutubia Central Legislative Assembly Agosti 1965. Mwalimu alisema hivi:

"... Nasisitiza tena kwamba Tanzania inaelewa matatizo ya kiuchumi ya jirani zake na inajutia utata wowote unaosababishwa na hitaji lake. Tumejaribu kuliepuka. Lakini tatizo letu lilidhihirika kwetu kabla ya uhuru wetu, hatukuchukua hatua mpaka 1964 kwa sababu tulitaraji suala hilo litashughulikiwa ndani ya mfumo wa Shirikisho la Afrika Mashariki. Kwa muda fulani tulikuwa tayari kukubaliana na hali iliyyo, na mapungufu yake yote dhidi yetu, kwa gharama ya umoja wa Afrika Mashariki. Lakini kwa kukosekana maendeleo au tumaini lolote la kuwa na shirikisho, tulikuwa hatuna njia nyingine bali kuangalia usawazishaji wa faida na hasara za soko la pamoja. Ni pale tu juhudi zetu ziliposhindwa kuleta makubaliano katika ngazi ya Afika Mashariki, ndipo kwa kusita, tukaamua kuchukua hatua binafsi..." [Tafsiri isiyo rasmi][3]

Mfululizo wa matukio yaliyofuatia yameandal wa kwa urefu kwenye makala nyingi zilizochambua kushindwa kuwepo ushirikiano madhubuti kwenye ukanda huu, hivyo hatutarudia mjadala huo. Kwa sasa yafaa tukumbushe kuwa wakati Tume ya Phillips inaundwa na kutoa mapendekezo yaliyopelekea kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki 1967, tofauti za kiitikadi zilishashamiri mno na yote yaliyojiri baadaye ni sehemu ya historia. Ufafanuzi huu mfupi wa kihistoria kwa sehemu kubwa umezungumzia kilichofanyika katika awamu ya kwanza ya uongozi wa nchi hii. Sehemu ifuatayo inatoa mwanga jinsi awamu zilizofuatia zilivyoyapa umuhimu masuala ya ushirikiano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

---

[2] Imetolewa kwenye makala yenye kichwa cha habari, ' Towards an East African Federation: Debate, Rationale and Declaration of June 1963" kwenye tovuti ya Kituo Cha Katiba; http://www.kituochakatiba.co.ug, kama ilivyotembelewa Mei 20; 2007.

[3] Ibid.

Serikali na Jumuiya ya Afrika Mashariki

Awamu ya Pili na Suala la Jumuiya

Wakati awamu ya pili ya uongozi wa nchi ilipoanza mwaka 1985 tayari nchi za Kenya, Tanzania na Uganda zilishawekeana makubaliano ya kugawana mali na madeni ya Jumuiya iliyovunjika mwaka 1977.Jambo moja zuri lililotokana na makubaliano hayo ya mwaka 1984 ni kipengele kilichozungumzia uwezekano wa kuanzisha ushirikiano baina ya nchi hizo tatu siku zijazo. Serikali ya awamu ya pili iliyoongozwa na Rais Mstaafu, Ali Hassan Mwinyi, ilifanya jitihada za kuweka mahusiano na jirani zake, haswa Kenya na Uganda, katika hali nzuri baada ya kukabiliwa na hali tete kwa vipindi fulani. Huo ulikuwa ni wakati ambapo yalifanyika mabadiliko ya uongozi katika nchi hizo na Tanzania ilikuwa inapitia kipindi kigumu sana kiuchumi. Jitihada za Serikali ya awamu ya pili hazikuishia hapo. Uongozi wa nchi ulikubali kukaa meza moja na majirani hao na kutoa taarifa ya pamoja iliyoonesha nia ya kufufua Jumuiya katika Mkutano wa Wakuu wa nchi tatu uliofanyika Nairobi Novemba 1991. Awamu hii ya uongozi pia ilifanikiwa kurudisha uhusiano mzuri na nchi jirani kama, Malawi, Zaire [sasa DRC], na Visiwa vya Komoro. Ni katika mazingira hayo ndipo Rais wa Malawi wakati huo, Kamuzu Banda, alifanya ziara ya kiserikali Oktoba 1991, kitu ambacho kisingedhaniwa kutokea kabla ya hapo (Kiondo, 1994).

Hivyo basi, muhula wa pili wa uongozi wa Rais Mwinyi ulitawaliwa si tu na mageuzi ya kisiasa [1992] na kiuchumi, bali pia pilika za kurejesha ushirikiano wa kikanda. Hatimaye pilika hizo ziliwezesha kusainiwa makubaliano ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki mnamo November 30, 1993. Mkataba wa makubaliano uliruhusu kuundwa kwa Tume ya Kudumu ya Nchi Tatu iliyojulikana kama Permanent Tripartite Commission ikipewa jukumu la kuratibu mchakato wa ushirikiano mpya. Je, baada ya Tanzania kufanya uchaguzi wake wa kwanza wa vyama vingi na kufanya mabadiliko ya uongozi, iliendelea kuyapa masuala ya Jumuiya msukumo unaostahili au ilidhoofisha msingi uliokwisha wekwa na awamu ya pili ya uongozi? Sehemu inayofuata inajibu swali hili.

Serikali na Jumuiya ya Afrika Mashariki

Awamu ya Pili na Suala la Jumuiya

Wakati awamu ya pili ya uongozi wa nchi ilipoanza mwaka 1985 tayari nchi za Kenya, Tanzania na Uganda zilishawekeana makubaliano ya kugawana mali na madeni ya Jumuiya iliyovunjika mwaka 1977.Jambo moja zuri lililotokana na makubaliano hayo ya mwaka 1984 ni kipengele kilichozungumzia uwezekano wa kuanzisha ushirikiano baina ya nchi hizo tatu siku zijazo. Serikali ya awamu ya pili iliyoongozwa na Rais Mstaafu, Ali Hassan Mwinyi, ilifanya jitihada za kuweka mahusiano na jirani zake, haswa Kenya na Uganda, katika hali nzuri baada ya kukabiliwa na hali tete kwa vipindi fulani. Huo ulikuwa ni wakati ambapo yalifanyika mabadiliko ya uongozi katika nchi hizo na Tanzania ilikuwa inapitia kipindi kigumu sana kiuchumi. Jitihada za Serikali ya awamu ya pili hazikuishia hapo. Uongozi wa nchi ulikubali kukaa meza moja na majirani hao na kutoa taarifa ya pamoja iliyoonesha nia ya kufufua Jumuiya katika Mkutano wa Wakuu wa nchi tatu uliofanyika Nairobi Novemba 1991. Awamu hii ya uongozi pia ilifanikiwa kurudisha uhusiano mzuri na nchi jirani kama, Malawi, Zaire [sasa DRC], na Visiwa vya Komoro. Ni katika mazingira hayo ndipo Rais wa Malawi wakati huo, Kamuzu Banda, alifanya ziara ya kiserikali Oktoba 1991, kitu ambacho kisingedhaniwa kutokea kabla ya hapo (Kiondo, 1994).

Hivyo basi, muhula wa pili wa uongozi wa Rais Mwinyi ulitawaliwa si tu na mageuzi ya kisiasa [1992] na kiuchumi, bali pia pilika za kurejesha ushirikiano wa kikanda. Hatimaye pilika hizo ziliwezesha kusainiwa makubaliano ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki mnamo November 30, 1993. Mkataba wa makubaliano uliruhusu kuundwa kwa Tume ya Kudumu ya Nchi Tatu iliyojulikana kama Permanent Tripartite Commission ikipewa jukumu la kuratibu mchakato wa ushirikiano mpya. Je, baada ya Tanzania kufanya uchaguzi wake wa kwanza wa vyama vingi na kufanya mabadiliko ya uongozi, iliendelea kuyapa masuala ya Jumuiya msukumo unaostahili au ilidhoofisha msingi uliokwisha wekwa na awamu ya pili ya uongozi? Sehemu inayofuata inajibu swali hili.

Awamu ya Tatu na Suala la Jumuiya

Awamu ya tatu iliyoongozwa na Rais Mstaafu, Benjamin William Mkapa iliingia madarakani mwaka 1995. Hiki ni kipindi ambacho Tanzania ilikuwa imebadili mfumo wa kisiasa baada ya Watanzania kushiriki uchaguzi mkuu uliohusisha vyama vingi. Serikali ya Mkapa ilikuta tayari mahusiano ya nchi tatu za Afrika Mashariki yako katika hali nzuri. Uongozi wa Mkapa ulikuta tayari awamu iliyopita imeonesha, kwa niaba ya Watanzania, dhamira ya dhati ya kufufua ushirikiano wa kikanda. Serikali ya Mkapa bado ilikuwa na changamoto ya kusukuma gurudumu la mchakato wa ushirikiano na hivyo kuthibitisha nia ya Tanzania kushirikiana na majirani zake. Kwa kweli ni wakati wa kipindi cha uongozi wa awamu ya tatu ndipo mambo mengi na hatua kubwa zihusuyo Jumuiya mpya ya Afrika Mashariki zilipochukuliwa. Mwezi Machi 1996 Sekretarieti ya Jumuiya ilianzishwa Arusha, ikifuatiwa na hatua ya kupitisha Mkakati wa Maendeleo [1997-2000]; kusainiwa kwa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki [Novemba 30, 1999], na kusainiwa Hati ya Ushuru wa Forodha [Januari 1, 2004]. Mwaka 2004, Rais Mkapa akakubaliana na Wakuu wenzake wa nchi kuunda Kamati [maarufu kama Kamati ya Wako] ya kuangalia uwezekano wa kuharakisha uundwaji wa shirikisho la Afrika Mashariki kama tulivyoeleza kwenye utangulizi wa makala hii. Ripoti ya Kamati ya Wako iliyowasilishwa kwenye Mkutano wa Sita wa Wakuu wa Nchi Novemba 26, 2004 inamnukuu Rais Mkapa akisema hivi kuhusu suala la Shirikisho ifuatayo:

> "Tuna kila namna ya kufaidika na Shirikisho la Afrika Mashariki kwa maana ya utulivu wa kisiasa, kujisikia salama na kama chombo cha kiuchumi chenye uwezo zaidi wa kupambana na umaskini." [Tafsiri isiyo rasmi] [Ripoti ya Kamati ya Wako, 2004:8]

Awamu ya Nne na Suala la Jumuiya

Wakati ushiriki wa Tanzania katika shughuli za Jumuiya ya Afrika Mashariki unashika kasi chini ya uongozi wa awamu ya tatu kiongozi wa awamu ya nne, Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje

kwa kipindi chote. Hivyo, alikuwa katika nafasi nzuri ya kufahamu mwenendo mzima wa Jumuiya na msimamo wa nchi yake katika mambo ya msingi ya ushirikiano huo wa kikanda. Ni kipindi hicho akitumikia wadhifa ya uwaziri wa mambo ya nje ndipo Tanzania ilipojivua uanachama wa Umoja wa Soko la Pamoja kwa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika (COMESA). Serikali ikaamua kutilia mkazo ushiriki wake kwenye ushirikiano wa kikanda wa SADC na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Serikali ya awamu ya nne imewajibika mara kadhaa kutoa msimamo wa kusisitiza kwamba Tanzania haifikiri kujiunga tena na COMESA kama baadhi ya wadau, wakiwemo wafanyabiashara wa ndani, wanavyolivalia njuga. Serikali ya awamu ya nne imelazimika kutoa msimamo wake kuhusu jambo hili baada ya kuonekana kuwepo shinikizo zisizo rasmi kutoka kwa nchi wanachama wengine wa Jumuiya kutaka ijiunge tena na COMESA.

Wakati Rais mstaafu wa awamu ya tatu alipokuwa anamtambulisha Rais Mteule Kikwete kwa wahisani, aliwahakikishia kuwa Rais wa Awamu ya Nne ataendeleza sera zilizoanzishwa na awamu iliyopita. Msimamo wa Tanzania katika shughuli za Jumuiya haukutarajiwa kubadilika kinyume na msingi uliokwisha wekwa na awamu ya tatu. Ikumbukwe kwamba hata pale ilipoamuliwa kuangalia uwezekano wa kuharakisha ujio wa shirikisho la Afrika Mashariki mwaka 2004 Tanzania ndiyo iliyotoa wazo la kuundwa kwa kamati za kukusanya maoni kwa nchi zote tatu. Awamu ya Nne ikalisisitiza na kusimamia msimamo wa Tanzania pamoja na kuhusisha gharama kubwa, kama ilivyothibitishwa na Rais Kikwete wakati alipokutana na Kamati ya kukusanya maoni kuhusu uharakishwaji wa kuanzisha Shirikisho kwa Tanzania iliyokuwa chini ya uenyekiti wa Profesa Samuel Wangwe. Rais alikaririwa akisema:

> "Wazo la kwamba tuwachie wananchi waamue kuhusu shirikisho lilikuwa ni wazo la Tanzania, wenzetu waliona tunapoteza wakati, waliona viongozi wanaweza kuamua tu kuwashirikisha wananchi wengi....Tanzania tulisema ngoja tuwashirikishe wananchi ili tupate uhakika kama wanaridhika na kuwa na shirikisho au la. Mimi naamini kwamba huu ndio utaratibu mzuri zaidi kuliko wa kuchukua maoni ya watu wachache..." (Mwingira, 2007).

Rais Kikwete alinukuliwa pia akiieleza Kamati ya Wangwe kwenye hafla

hiyo kuwa Nchi Mwanachama mmoja wa Jumuiya alifikia hatua ya kuandaa rasimu ya muundo wa Shirikisho bila ya kushirikisha wanajumuiya wengine. Akiendelea kueleza yaliyojiri Rais Kikwete alisema, "Tulipogundua hili, Rais Mkapa akanituma mimi wakati huo nikiwa Waziri wa Mambo ya Nje kwenda Kenya na Uganda, tukawaeleza wenzetu. Jamani hapana, hivi sivyo tunavyotakiwa kwenda. Tukawapa somo, hatimaye wakatuelewa... Lakini wenzetu waliona kuwaachia wananchi waamue ni kama vile viongozi tulikuwa tunajivua madaraka" (Mwingira, ibid.). Inaonekana kwamba Rais alilazimika kutoa ufafanuzi huo baada ya kutokea hoja ya kuwa hatua ya kuunda Kamati ya Wangwe ni kinyume na matakwa ya Katiba. Kiongozi wa chama cha siasa cha ushindani cha NCCR-Mageuzi, James Mbatia, alinukuliwa akieleza kuwa washauri wa Rais walimpotosha kuunda Kamati ya kukusanya maoni kuhusu suala nyeti la Shirikisho ambalo litahusisha kutwaa sehemu ya mamlaka ya nchi kwa chombo cha ushirikiano baina ya nchi.[4] Hoja iliyowasilishwa ni kuwa hatua hiyo ya Rais 'imeteka' mamlaka ya Bunge. Hoja hii ilijibiwa na Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Mary Nagu, na pia Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Samwel Sitta, kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano inamruhusu Rais kufanya mambo mengi ikiwemo kuunda Kamati na Tume za kukusanya maoni (Guardian, Januari 27, 2007).

Vyama vya Siasa, Wanasiasa, Masuala ya Jumuiya na Hoja ya Shirikisho

Kama tulivyoeleza hapo juu mfumo wa kisiasa wa Tanzania umetawaliwa na vyama vya siasa. Hivyo basi, linakuwa si jambo geni pale vyama na wawakilishi wao wanapokuwa mstari wa mbele ama kujihusisha au kutoa misimamo yao kuhusu mambo yahusuyo Jumuiya, na hususan suala hili la Shirikisho. Si lengo la sehemu hii kutoa tathmini ya awali ya maoni yaliyokwisha tolewa. Hapa tunajaribu kutazama suala moja kuu, nalo ni nafasi ya wanasiasa wa Tanzania kwenye Jumuiya yenyewe.

---

[4] Nakala ya kimaandishi ya taarifa ya Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, James Mbatia, ilinakiliwa kwa Spika wa Bunge la Jamhuri, Samwel Sitta, na kwa Jaji Mkuu, Barnabas Samatta.

Kama ilivyo kwa nchi wanachama wengine Tanzania inapewa fursa ya kuwakilishwa kwenye taasisi mbalimbali za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wawakilishi wako wa aina mbili; watendaji ndani ya Sekretarieti na wanasiasa kwenye chombo cha Jumuiya cha kutunga sheria, yaani Bunge la Afrika Mashariki. Kuwa mwakilishi wa Tanzania kwenye Jumuiya si tu ni moja ya dhamana nzito bali pia hutoa fursa ya kujijenga kisiasa. Tunachowakilisha hapa ni kuwa Jumuiya pekee bado haijafikia kuwa ni "jukwaa" linalojitegemea kwa wanasiasa wa Tanzania. Jumuiya imekuwa ni jukwaa la pili kwa lile jukwaa la kisiasa la kitaifa. Maana yake ni kuwa wanasiasa wetu ama wamelipanda au kulishuka jukwaa la kitaifa kwa kupitia jukwaa la Jumuiya. Wako walioiwakilisha nchi kama wabunge kwenye Jumuiya na baadaye kufanikiwa kuwa Wabunge ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano. Vilevile wako waliowahi kuwa Wabunge kwenye majimbo ya uchaguzi ambao wamefanikiwa kuwa Wabunge wa Afrika Mashariki.

Hali hii inasababishwa na sababu zifuatazo: kwanza, kiutaratibu kwa sasa Wabunge wa Jumuiya hawachaguliwi moja kwa moja na wananchi wa Afrika Mashariki. Mamlaka ya nani aiwakilishe Tanzania na kwa tiketi ya chama gani cha kisiasa ipo chini ya Wabunge wa Bunge la nchi. Zaidi ya hiyo ni kwamba mustakabali wa uwakilishi upo kwenye chama chenye viti vingi bungeni. Hatma ya mgombea wa kiti cha ubunge wa Jumuiya inadhihirika zaidi kuwa chini ya Mbunge wa Jamhuri ya Muungano na Baraza la Wawakilishi pale wanaofanya uchaguzi huo wanapopiga kura kama 'kundi' (block). Pili, hivi sasa kumeundwa wizara maalum inayoshughulikia masuala ya Jumuiya. Hatua hii haondoi umuhimu wa nafasi ya mbunge wa Afrika Mashariki bali inapunguza uwanja mpana aliokuwa nao mbunge kushughulikia mambo ya Jumuiya na hivyo kujijenga kisiasa. Itakumbukwa kuwa Bunge la Afrika Mashariki linaundwa na wabunge 27, ambapo kila nchi hutoa wabunge 9. Aidha kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi wa wabunge wa Afrika Mashariki, wabunge hutoka miongoni mwa vyama vyenye wabunge tu, ambavyo viko vitano. Kanuni za Bunge na Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinataka uwakilishi uzingatie uwiano wa vyama ndani ya Bunge.

Tumerejea masuala haya ya kanuni kwa kuwa kulikuwepo malalamiko

haswa toka kwa wanasiasa wa kambi ya upinzani kuhusu utaratibu wa kupata uwiano wa viti vya Bunge la Afrika Mashariki. Katika mchakato wa kupata wawakilishi wa sasa wa Tanzania kambi ya upinzani ilitengewa nafasi moja kati ya tisa. Kambi ya upinzani haikupendezwa na hali hiyo licha ya kuongeza viti vyake vya Bunge kutoka 17 mwaka 2001 mpaka 45 mwaka 2006. eneo lingine lililoibua mjadala kisiasa ni uwakilishi wa Zanzibar kwenye Bunge la Afrika Mashariki. Kwenye Bunge hilo nafasi tatu zimetengwa kwa Zanzibar. Kambi ya upinzani ilionyesha kutofurahishwa na utaratibu wa kushindanisha wanachama wa Chama cha Mapinduzi (CCM) pekee kuchukua nafasi hizo pamoja na Chama cha Wananchi (CUF) kukalia viti vyote vya Bunge na Uwakilishi vya moja ya visiwa viwili vinavyounda Zanzibar.

Duru za ndani za kisiasa pia ziligusia kwa kiasi fulani, zaidi kupitia baadhi ya magazeti yanayochapishwa nchini, kuzungumzia na kuchambua wasifu wa wagombea wa ubunge wa Afrika Mashariki. Wakati huu wasifu binafsi wa wagombea, si tu wa kambi ya upinzani bali pia wa Chama Tawala ulipata mvuto wa aina yake. Kwa bahati mbaya, uchambuzi wa kina wa suala hilo uko nje ya makusudio ya makala hii.

Uwakilishi na ubunge ni miongoni mwa nafasi adhimu sana katika ulingo wa kisiasa nchini. Hata pale Mwakilishi au Mbunge anapokaribishwa kutoa maoni yake binafsi kuhusu Shirikisho la Afrika Mashariki anachokizungumza kinachukuliwa kwa makini na wapiga kura wake. Hata pale ilipotolewa msisitizo kuwa maoni ya wabunge hayawakilishi wakazi wa majimbo yao wakati wa kukusanya maoni yao nje ya vikao vya kawaida vya Bunge, baadhi yao walisikika wakidai "wananchi wa jimbo langu wanasema hivi..."(Sunday Observer; Majira , Aprili 22, 2007). Hawa walifanya hivyo wakijua nafasi ya kisiasa aliyonayo Mbunge na uwezo wa ushawishi katika jamii anayoiwakilisha. Kwa maana nyingine inakuwa vigumu kwa mwananchi wa kawaida kutofautisha mawazo binafsi ya mwanasiasa, kwa upande mmoja, na pale anapotumia nyadhifa aliyonayo kuwakilisha maoni. Wanasiasa wametoa maoni yao kuhusu Shirikisho na hofu walizonazo katika masuala mbalimbali yakiwemo yanayohusu ardhi, ajira, viwango vya elimu, ukubwa na udogo wa sekta za biashara na uchumi, vurugu za kisiasa,

haswa toka kwa wanasiasa wa kambi ya upinzani kuhusu utaratibu wa kupata uwiano wa viti vya Bunge la Afrika Mashariki. Katika mchakato wa kupata wawakilishi wa sasa wa Tanzania kambi ya upinzani ilitengewa nafasi moja kati ya tisa. Kambi ya upinzani haikupendezwa na hali hiyo licha ya kuongeza viti vyake vya Bunge kutoka 17 mwaka 2001 mpaka 45 mwaka 2006. eneo lingine lililoibua mjadala kisiasa ni uwakilishi wa Zanzibar kwenye Bunge la Afrika Mashariki. Kwenye Bunge hilo nafasi tatu zimetengwa kwa Zanzibar. Kambi ya upinzani ilionyesha kutofurahishwa na utaratibu wa kushindanisha wanachama wa Chama cha Mapinduzi (CCM) pekee kuchukua nafasi hizo pamoja na Chama cha Wananchi (CUF) kukalia viti vyote vya Bunge na Uwakilishi vya moja ya visiwa viwili vinavyounda Zanzibar.

Duru za ndani za kisiasa pia ziligusia kwa kiasi fulani, zaidi kupitia baadhi ya magazeti yanayochapishwa nchini, kuzungumzia na kuchambua wasifu wa wagombea wa ubunge wa Afrika Mashariki. Wakati huu wasifu binafsi wa wagombea, si tu wa kambi ya upinzani bali pia wa Chama Tawala ulipata mvuto wa aina yake. Kwa bahati mbaya, uchambuzi wa kina wa suala hilo uko nje ya makusudio ya makala hii.

Uwakilishi na ubunge ni miongoni mwa nafasi adhimu sana katika ulingo wa kisiasa nchini. Hata pale Mwakilishi au Mbunge anapokaribishwa kutoa maoni yake binafsi kuhusu Shirikisho la Afrika Mashariki anachokizungumza kinachukuliwa kwa makini na wapiga kura wake. Hata pale ilipotolewa msisitizo kuwa maoni ya wabunge hayawakilishi wakazi wa majimbo yao wakati wa kukusanya maoni yao nje ya vikao vya kawaida vya Bunge, baadhi yao walisikika wakidai "wananchi wa jimbo langu wanasema hivi..."(Sunday Observer; Majira , Aprili 22, 2007). Hawa walifanya hivyo wakijua nafasi ya kisiasa aliyonayo Mbunge na uwezo wa ushawishi katika jamii anayoiwakilisha. Kwa maana nyingine inakuwa vigumu kwa mwananchi wa kawaida kutofautisha mawazo binafsi ya mwanasiasa, kwa upande mmoja, na pale anapotumia nyadhifa aliyonayo kuwakilisha maoni. Wanasiasa wametoa maoni yao kuhusu Shirikisho na hofu walizonazo katika masuala mbalimbali yakiwemo yanayohusu ardhi, ajira, viwango vya elimu, ukubwa na udogo wa sekta za biashara na uchumi, vurugu za kisiasa,

mamlaka za dola, gharama za zoezi lenyewe la kukusanya maoni, mlinganuao wa miundo ya kiutawala, utamaduni, kodi na ushuru wa forodha, uzoefu wa Umoja wa Ulaya, na mambo mengine kadhaa. Kwa hakika hatuwezi kusema kuwa mitazamo ya wanasiasa katika mambo hayo haitakuwa na athari hasi au chanya kwenye fikra za wananchi watakaobahatika kutoa maoni kwa Kamati ya Wangwe.

Mitazamo Kuhusu Zanzibar na Hoja ya Shirikisho

Tanzania ni Jamhuri ya Muungano yenye kuunganisha iliyokuwa Tanganyika na Zanzibar. Hoja ya Shirikisho la Afrika Mashariki imetawala duru za kisiasa za Tanzania wakati ambapo pande mbili za Muungano ziko katika mchakato wa kuzitafutia suluhu kero za muungano[5] huo, na wakati huo vyama viwili vyenye upinzani na ufuasi mkubwa visiwani vikiwa katika meza ya mazungumzo kushughulikia kile kinachoelezwa kama 'mpasuko' wa kisiasa katika eneo hilo. Ujio na kutawala kwa hoja ya shirikisho nchini kumekuwa kama ni faraja kwa baadhi ya Watanzania kwani kumewapa fursa ya ziada ya kuujadili muungano. Hoja ya Shirikisho imetoa tiketi ya kutoa dukuduku si tu kuhusu Muungano bali pia nafasi ya Zanzibar katika Jumuiya iliyopo ya Afrika Mashariki. Kwa ufupi, mambo makuu mawili yamejitokeza katika duru za kisiasa. Jambo la kwanza ni uanachama wa Zanzibar kwenye Jumuiya. Suala hili limejitokeza na kupewa ufafanuzi ndani ya Baraza la Wawakilishi na Bunge la Jamhuri ya Muungano. Akijibu hoja za wajumbe waliotaka ufafanuzi wa kwa nini Zanzibar sio mwanachama wa kujitegemea katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), Idd Pandu Hassan, alikaririwa akisema Zanzibar haiwezi kuwa mwanachama kwa vile haina sifa za utaifa. (Sadallah, Januari 25, 2007) Ufafanuzi kama huo ulitolewa na Mbunge wa Donge (CCM), Ali Ameir Mohamed ambaye pia

[5] Kero zilizokwisha jadiliwa katika vikao vya pamoja ni ugawanaji wa mapato yatokanayo na misaada kutoka nje ya nchi, faida ya Benki Kuu na Mikopo, Malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili, Utekelezaji wa Sheria ya Tume ya Haki za binadamu, Utafutaji na Uchimbaji Mafuta na Gesi, na Uvuvi katika Bahari ya Hindi.

ni mjumbe wa Tume ya kukusanya maoni juu ya kuharakishwa uanzishaji Shirikisho la Afrika Mashariki. Naye Naibu Waziri katika Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dkt. Diodorous Kamala aliwajibika kutoa ufafanuzi bungeni kwa swali la mbunge aliyetaka kufahamu kiwango cha ada ya uanachama kinacholipwa na Zanzibar. Naibu Waziri alisema Mkataba wa Jumuiya unaitambua Zanzibar kama sehemu ya Tanzania, hivyo hailazimiki kulipa ada (Thomas, 2007). Hata baada ya ufafanuzi huo, maoni ya Zanzibar kupewa fursa ya uanachama wa kujitegemea yaliendelea kutolewa wakati wa semina ya uhamasishaji wananchi kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyofanyika Bwawani Hotel, Zanzibar mwezi Machi 2007.

Suala la pili ni kero za Muungano, likihusishwa na suala la Shirikisho. Wapo waliotumia fursa ya kuizungumzia Jumuiya na mustakabali wake kwa kukumbusha kero zilizopo za Muungano. Hapa kuna makundi makuu mawili. Wako wenye maoni kuwa kero za Muungano zitatuliwe kwanza kabla ya Tanzania kuingia katika Shirikisho la Afrika Mashariki.[6] Wako pia wale wanaotazama maslahi ya Zanzibar kwa ujumla yalivyo sasa katika Jumuiya hata kabla ya kufikia Shirikisho lenyewe. Wanaoangukia kundi hili wanatazama zaidi sekta za uchumi na biashara. Katika Semina kuhusu Jumuiya tuliyokwisha itaja hapo awali, mmoja wa wachangiaji alikuwa ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais anayeshughulikia Fedha na Uchumi, Zanzibar, Dk. Mwinyihaji Makame Mwadini, ambaye "alieleza kuwa suala la ushuru katika nchi wanachama wa Afrika Mashariki linahitaji kuangaliwa kwa umakini mkubwa kwa kuwa Zanzibar haitanufaika na sheria ya kulinda biashara inayozalishwa ndani kama ilivyopitishwa katika Jumuiya hiyo...Waziri Makame alisema "Zanzibar inategemea bidhaa za unga, mchele na sukari kutoka nje ya nchi na kama itatumia bidhaa hizo kutoka nchi wanachama wa Jumuiya hiyo wananchi wataumia kwa vile zinauzwa kwa bei kubwa ikilinganishwa na zile zinazotoka nje ya nchi..." (Sadallah, 2007).

6 Maoni kama hayo yametolewa na Rais wa Chama cha Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Wakulima Zanzibar, kwenye Semina ya kuhamasisha kuhusu Jumuiya, Mwezi Machi 2007. kwa taarifa zaidi tazama Nipashe, Machi 17, 2007.

Ujumbe tunaoupata hapa ni kuwa Watanzania wanapojadili suala la Shirikisho la ukanda wa Afrika Mashariki wasiangalie tu utambulisho wa kisiasa bali pia maslahi ya kiuchumi. Kwa maana nyingine, wadau waichambue hoja ya shirikisho kwa darubini pana zaidi ya hofu ya kumezwa au kupoteza utambulisho wa kisiasa na kutathmini kwa tahadhari kubwa maslahi ya kiuchumi na biashara. Mwanasiasa yeyote makini na mwadilifu aliyepewa dhamana ya kumwakilisha mpiga kura kwenye mamlaka za kiutawala daima atakuwa na wasiwasi wa matokeo ya ama kutotetea, kutokusimamia, au kutokuendeleza maslahi ya wapiga kura.

Hitimisho

Makala hii imejaribu kuibua mjadala wa hoja ya Shirikisho la Afrika Mashariki ilivyogusa duru za kisiasa rchini, sehemu kubwa ikitumia mtazamo wa kihistoria, lakini pia kwa mtindo wa kuweka mlinganuo wa masuala na matukio yaliyojiri na yenye uhusiano na mada kuu. Mjadala uliojitokeza umeibua mambo makuu matano, miongoni mwa mengine mengi. Moja, ni wazi kuwa muktadha wa kisiasa uliokuwepo miaka ya sitini ni tofauti na wa sasa. Duru za kisiasa zilipigia chepuo hoja ya Shirikisho kiasi kwamba ilionekana wazi kuwa ujumbe wa kisiasa toka Tanzania ni Shime Wana-Afrika Mashariki twendeni kwenye Shirikisho. Muktadha wa sasa wa kisiasa umelazimu ukusanyaji wa maoni ya wadau kwanza kabla ya kutoa ujumbe wa kisiasa kutoka kwa Watanzania kuhusu Shirikisho. Makala hii haina fursa ya kutoa utabiri kama ujumbe huo utakuwa kama wa miaka ya sitini au utakuwa ni wa kutaka kuchelea Shirikisho.

Pili, hatua za makusudi na madhubuti zimechukuliwa kurudisha mahusiano mazuri na majirani zetu, kisha kufufua Jumuiya, na kushiriki kuunda taasisi na programu mbalimbali za Jumuiya mpya ya Afrika Mashariki katika awamu ya pili mpaka ya nne ya uongozi wa Serikali ya Tanzania. Pia imedhihirika kuwa serikali ya Tanzania ndiyo iliyofanya ushawishi wa kukusanya maoni ya wananchi wa ukanda huu kuhusu hoja ya kuharakisha Shirikisho aula. Tatu, kama ilivyoonekana katika sehemu ya pili ya makala hii, hali ya duru za ndani za kisiasa kutawaliwa na vyama vya siasa inepenyeza mpaka kwenye hoja ya Shirikisho na masuala ya

Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ujumla. Kinyang'anyiro cha uteuzi wa wabunge wa Jumuiya kimeendelea kuleta mvuto zaidi wa tiketi ya vyama vyenye uwakilishi Bungeni zaidi ya umahiri na mrengo wa kisiasa wa wagombea wenyewe. Maoni ya binafsi ya wabunge waliopata fursa ya kutoa maoni yao kuhusu hoja ya Shirikisho yalivuka uzio wa vyama pale baadhi yao walipodai 'wametumwa' na wapiga kura wao waseme kile walichosema. Hali hiyo ilipelekea Serikali kutoa ufafanuzi kuwa maoni ya Wabunge hayawakilishi Bunge wala majimbo yao. Kwa mtazamo wetu ni vigumu kuweka bayana tofauti ya Mbunge kama Mbunge na kama raia mwingine kwenye masikio na mioyoni mwa mwananchi wa kawaida. Nne, zoezi la kukusanya maoni kuhusu Shirikisho limekuwa kama "nafasi ya dhahabu" kwa Watanzania wa nyanja tofauti za maisha kuujadili muungano na maslahi ya Zanzibar kwenye Jumuiya na hatimaye Shirikisho. Si wanasiasa na viongozi tu waliotumia fursa iliyopo kuhimiza haja ya kushughulikia 'kero' za muungano kwanza kabla ya kutoa uamuzi wa kuingia kwenye Shirikisho, bali pia wananchi wa kawaida. Aidha, ujumbe uliojitokeza ni kuwa wadau wanafuatilia kwa tahadhari hoja ya Shirikisho na masuala mengine ya Jumuiya kwa kutilia maanani maslahi ya kiuchumi na kibiashara ya wapiga kura.

Huu ni utambulisho muhimu katika nyakati hizi za ushirikiano wa jumuiya za kikanda sambamba na utambulisho wa kisiasa na nembo nyingine za kitaifa. Na tano, bado kuna uelewa mdogo wa masuala ya Jumuiya iliyopo sasa. Hali hii imelazimu kuendeshwa kwa programu ya kutanabahisha shughuli za Jumuiya pamoja na umuhimu wake. Kufikia fursa hii haturia budi kurejea sehemu ndogo ya uchambuzi wa masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanywa mwaka 1977 msomi na mwanadiplomasia, Augustine P. Mahiga, kwamba, "ushirikiano wa Jumuiya ya kikanda ambao unashughulikia dhana ya kutoendelea lazima itilie maanani mawazo na kiwango cha uelewa wa dhana yenyewe miongoni mwa nchi wanachama. Jumuiya ya Kikanda haitaweza kuwepo kama itangojea mpaka wanachama wote wafikie kiwango kimoja cha uelewa wa dhana na tafsiri ya kutoendelea..." (tafsiri yetu). Tunachoongeza hapa ni swali kuwa je kipo kiwango gani cha uelewa cha Watanzania kuhusu hoja ya Shirikisho na hicho kiwango kinalinganishwa vipi na uelewa wa viongozi wao?

Marejeo

Chaligha, A. *et. al.* (2002). "Uncritical Citizens or Patient Trustees? Tanzanians' Views of Political and Economic Reform", Afrobarometer Working Paper No. 18. A comparative series of national public attitude surveys on democracy, markets and civil society in Africa.

Daniel, J. (2007). "Wabunge Nao Wakataa Shirikisho Afrika Mashariki: Wahoji siri iliyojificha, Wataka Kikwete asimamishe Tume, Mbunge aonya tukikubali, Nyerere anaweza 'Kufufuka'", *Majira*, Aprili 22.

East African Community, (2004). Report of the Committee on Fast Tracking East African Federation, submitted to the Sixth Summit of Heads of State of the East African Community, Arusha, 26th November.

Guardian, Tanzania Daily, January 01, 2007. "Sita astonished by Mbatia's Remarks?"

http://www.kituochakatiba.co.ug, Tovuti ya Kituo cha Katiba: Eastern Africa Centre for Constitutional Development.

Kassum, A. (1977). "The Future of the East African Community," *UTAFITI*, Vol. 11 No. 1 pp.5-23.

Kiondo, A. (1994). " Tanzania's Foreign Policy: The Socio-Economic Context," in W. Oyugi [ed.], *Politics and Administration in East Africa*, Nairobi: East African Educational Publishers.

Mahiga, A. (1977). "The Pitfalls and Promises of Regional Integration in East Africa," *UTAFITI*, Vol. 2. No.1, pp. 25-44.

Mmuya, M. (2002). "Hali ya Vyama vya Siasa Tanzania", in J. Madumulla [ed.], *Uimarishaji Demokrasia na Utawala wa Kidemokrasia Tanzania*, REDET Publication.

Mukandala, R. and Killian, B. 2004. "Political Cooperation in East Africa", in S. Mushi *et. al.* [eds.] *Democracy and Social Transformation in East Africa*, REDET Publication.

Mushi, S.S. (2001). "Political Tolerance in Tanzania's Culture" in *Tanzania's Political Culture: A Baseline Survey*, Dar es Salaam Dar es Salaam University Press.

Mwingira, M. (2007). "Kikwete: Tulishinikiza Wananchi Ndio Waamue," *Nipashe*, Februari 5.

Nyirabu, M. (2002). "The Multiparty Reform Process in Tanzania: The Dominance of the Ruling Party", *African Journal of Political Science*, Vol. 7, No.2.

Nyerere, J. (1966). *Freedom and Unity: A Selection from Writings and Speeches, 1952-65*, Dar es Salaam: Oxford University Press.

Sadallah, M. (2007). "Tatueni Kero za Muungano Kabla ya Shirikisho", *Nipashe*, Machi 17.

Sadallah, M. (2007). "Zanzibar Haiwezi Kuwa Mwanachama Anayejitegemea", *Nipashe*, Januari 25.

Sebalu, P. (1972). The East African Community, *Journal of African Law*, 16(3): pp.263-345.

Semaya, A. (2007). " Uelewa Mdogo Tatizo Ukusanyaji Maoni", *Habari Leo*,Jumapili, Aprili 8.

Tarrosy, I. (2005). "Past Fears-Future Hopes, An Example for Regional Co-operation Outside Europe: From the East African Community to an East African Federation", in I. Tarrosy and G. Rosskogler [eds.], Regional Cooperation as Central European Perspective, Proceedings of the 1st DRC Summer School Pecs: Europe Centre Pbc.pp. 161-169.

Thomas, J. (2007). " EAC Membership Fee is Not a Must for Zanzibar", Guardian, Aprili 13.

Thomas, J. (2007). "Go Slow on Federation. MPs Caution", Sunday Observer, Dar es Salaam, Aprili 22.